



Swahili
Colloquium
Bayreuth



UNIVERSITÄT
BAYREUTH

Kongamano la Kiswahili la 38

Bayreuth, tarehe 15 Mei hadi 17 Mei 2026

Wapendwa washiriki,

Tuna furaha kukualikeni kuadhimisha pamoja nasi Kongamano la Kiswahili la thelathini na nane mjini Bayreuth!

Tangu hapo mwaka wa 1987, ambapo kongamano la kwanza lilifanyika ili kusherehekea miaka 100 ya ufundishaji wa Kiswahili vyuoni nchini Ujerumani, Kongamano la Kiswahili limepiga hatua nyingi. Kongamano letu ni jukwaa la kipekee linalofanyika kila mwaka katika chuo kikuu cha Bayreuth. Mkutano huu unajumuisha jamaa kubwa ya kimataifa ya wasomi na watafiti wa taaluma mbalimbali ambao wanachunguza vipengele kadha wa kadha vya lugha ya Kiswahili, fasihi na tamaduni mahususi za Afrika Mashariki barani Afrika na ughaibuni. Mitazamo inayojikita katika nyanja mbalimbali pamoja na michango anuwai kutoka masomo ya kiisimu au kifasihi hadi anthropolojia na historia ndicho kipengele kinachodhihirisha upekee wa Kongamano hilo. Tutafurahi kuwakaribisha tena wote ambao huhudhuria Kongamano katika miaka iliyopita na pia tutafurahi kuwapokea washiriki wapya katika kongamano lijalo.

Mada kuu ya Kongamano la Kiswahili la 38

Kongamano la 38 la Kiswahili litakuwa na mada ya “**Sauti za Maana**”. “Sauti” inaweza kuchukuliwa kuwa na maana tofauti: Kwanza, sauti ya mtu inayotoka mdomoni mwake ama ya chombo, kama ala za muziki. Kwa hivyo, sauti kwa maana hiyo inatia mkazo kwenye muziki ama usimulizi. Vilevile kwa maana pana zaidi ama ya kisitiari, sauti inaweza kumaanisha mtazamo. Na kwa hivyo sauti inaweza kusafirisha maana ama sauti yenyewe inaweza kuwa na maana.

Polisemia ya sauti za maana ndiyo inayoashiria vipengele vitatu vya sauti ambavyo Kongamano letu litadhamiri kuchunguza.

Kwanza, tunajiuliza, je, kwa njia gani wingi wa aina za muziki wa Kiswahili zimekuwa vifaa vya kiubunifu vya kutoa maana mbadala? Tofauti na maandishi yaliyochapishwa, ambayo mara nyingi yanachukuliwa huweka vizingiti na hufungamana na udhibiti wa kikanuni wa mfumo fulani kama elimu rasmi kwa mfano, na ambayo husomwa na sehemu ndogo tu ya watu wa Afrika Mashariki, muziki – iwe taarab, Bongo fleva au hip-hop – ndio nyenzo pekee za kustawisha ubunifu wa lugha ya Kiswahili. Ni katika maneno ya nyimbo ambapo sauti za kupinga kauli za kiudhibiti, za kutetea haki za watu dhidi ya wenye nguvu na madaraka, za kuonyesha maovu na upungufu katika jamii na kupigania ndoto za jamii zinajitokeza na hata tafakuri za kifalsafa za kuwako. Aidha, muziki hutoa pia hazina mbadala ya maarifa licha ya masimulizi ya kawaida juu ya historia na kumbukumbu za kitamaduni.

Pili, mbali na kuchanguanua matini, yaani lugha katika muziki na kusoma maneno yake tu, Kongamano la Kiswahili linakusudia hususan kupekua sauti ya lugha na ya muziki yenyewe. Muziki na usimulizi haziundi maana tu kwa kutumia lugha na maneno, bali pia kupitia sauti zake zinazofikia hisia moja kwa moja. Ni kupitia sauti za muziki zinazogusa hisia kwamba muziki ukawa chombo chenye nguvu cha kutoa maana juu ya jinsi watu wanavyofahamu utambulisho wao, mwelekeo wao, mahali, historia na wakati wao. Kwa njia gani maonyesho na matendo ya muziki huunda dhana za jamii mpya na namna za kushirikiana mpya? Kwa jinsi gani uhusiano wa karibu wa sauti za muziki wa Kiswahili na aina nyingine za muziki wa Bahari ya Hindi huunda hisia za kutegemeana na kushirikiana?

Tatu, tunalenga kujadili mgawanyiko baina ya matini andishi na simulizi na kutilia mkazo tendo la kusimulia, kughani na kusikiliza fasihi – kuanzia fasihi simulizi hadi *slam poetry*. Katika miktadha mingi ya Afrika Mashariki, iliyo na historia ndefu ya masimulizi, hali ya kukariri, kunena na kuimba imepewa kipaumbele zaidi ya kusoma na kuandika. Na ndicho kitu kinachothaminiwa sana sio kama sanaa ya mdomo tu, bali kama njia muhimu ya uzalishaji maarifa pia. Pwani ya Kiswahili pamoja na tamaduni nyingi za bara zimeshuhudia kuendelezwa kwa aina mbalimbali za bahari za kujibizana zilizotoholewa kwenye njia za mawasiliano na fani anuwai, kama vile ngonjera iliyosifu itikadi ya ujamaa wakati wa miaka ya sitini, au malumbano ya vipindi vya redio, kanda na siku hizi mitandao ya kijamii. Kila chombo kimefungua mwenendo mpya wa kughani, kunena, kuimba na kutenda na kusikia na kusikiliza vile vile. Hivi karibuni miradi ya utafiti kadha imehusisha ukariri/usimulizi wa matini kama sehemu muhimu ya uchambuzi wa matini. Kulingana na juhudi za ubunifu zinazoshamiri kuunganisha miradi ya vitabu na uchambuzi wake na kukariri pamoja na muziki, hivyo basi tunaalika michango inayochambua kipengele cha mdomo na sauti kama njia ya kutoa maana katika matini mbalimbali kama za fasihi, mahubiri ya kidini au hotuba za kisiasa.

Kwa Kongamano la Kiswahili la 38 tunakaribisha michango inayojishughulisha na sauti na maana zake nyingi kwa mitazamo ya kiuhakiki na kiubunifu. Dhima za njia za mawasiliano, tanzu, wahusika na aina

za kutoholewa na kukopa mitindo ya muziki bado zitachukua nafasi kubwa katika jamii za Afrika Mashariki. Tuna uhakika kwamba Kongamano la Kiswahili, lililo jukwaa la taaluma nyingi, linaweza kutoa uwanja wa kipekee wa kujadiliana sauti kama mtazamo/fikra, kwa upande mmoja, na sauti za muziki na usimulizi, kwa upande mwingine, ili kuvuka mipaka ya mgongano baina ya lugha au matini, na muziki na usimulizi.

Usajili

Tutapokea michango kwa Kiswahili na Kiingereza. Kila wasilisho litapewa muda wa dakika thelathini; ambamo dakika ishirini ni za kuwasilisha na dakika kumi ni za majadiliano na hadhira. Tafadhalini mjiandikishe kwa baruapepe kupitia swahili@uni-bayreuth.de na mtutumie kichwa cha makala au mapendekezo ya paneli pamoja na ikisiri fupi isiyozidi maneno 250 mpaka tarehe 10 Januari 2026. Iwapo mtawasilisha kwa Kiswahili, tutumie pia muhtasari wa makala kwa Kiingereza. Tunawaomba wote kujiandikisha hata ikiwa mtashiriki bila ya kuwasilisha makala, ili tuweze kupanga vizuri.

Wakati/Mahali

Kongamano litafanyika kuanzia tarehe 15 Mei hadi 17 Juni mwaka 2026, Chuo Kikuu cha Bayreuth.

Tutatoa taarifa zaidi kuhusu Kongamano hapo baadaye. Pia, endapo kuna maswali yoyote usisite kuwasiliana nasi kwa barua pepe hii, swahili@uni-bayreuth.de

Karibuni nyote!

Salamu nyingi kutoka Bayreuth,

Watayarishaji wa kongamano

Serena Talento na Clarissa Vierke

Swahili Colloquium

Literaturen in afrikanischen Sprachen

Universität Bayreuth

95440 Bayreuth

Telefon: + 49 921 55-3550

Fax: + 49 921 55-3641

Email: swahili@uni-bayreuth.de

http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq/